## DUNIA KITENDAWILI

*O. McOnyango*

Masika na Ukame
Misitu na Majangwa
Ndivyo mambo yalivyo.

Watu wote njia moja,
Sivyo mambo yakuwavyo.

Kulia na Kushoto
Kushoto na Kulia
Basi Kulia ni Kushoto
Na Kushoto ni Kulia
Ndivyo mambo yakuwavyo.

Mpanda ngazi hushuka
yawezekana
Mpanda ngazi kupanda
pia

Mshuka ngazi hupanda
tahadhari!
Mshuka ngazi hushuka.
Mara kwa mara,

Ngazi hupanda na kushuka!
Ndivyo mambo yalivyo.

Kuwa bikira, huko ndiko kutakata
Kuzaa bikira, ni lazima kuwa taka!!!

Kurudirudi ndiko kwenda!
Huo ndio Ulimwengu.